

**KUMB: PPR/18 - 05/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUENZIA JUMATANO, TAREHE 2 MEI 2018**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 2 Mei 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchini, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Aprili 2018. Kwa mwezi Mei 2018, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 88/lita (sawa na asilimia 3.80) na Shilingi 61/lita (sawa na asilimia 2.75), sawia, wakati bei za Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 2/lita (sawa na asilimia 0.09). Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 100.91/lita (sawa na asilimia 4.58), Shilingi 73.71/lita (sawa na asilimia 3.52) na Shilingi 10.49/lita (sawa na asilimia 0.51) sawia. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwenye soko la ndani yametokana na kushuka kwa bei za mafuta hayo katika soko la dunia na kupungua kwa gharama za usafirishaji wa mafuta (*BPS Premium*). Vilevile, mabadiliko ya bei yamechangiwa na kubadilika kwa Kanuni ya Kukokotoa Bei za Mafuta nchini ili kujumuisha gharama kwa Wakala za Serikali na tozo za huduma za Manispaa na Jiji kwa wauzaji wa mafuta kwa jumla na rejareja.
- (b) Hakuna mzigo mpya wa mafuta uliopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga kwa mwezi wa Aprili 2018. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya Kanuni za Kukokotoa Bei za Mafuta nchini, bei za jumla na rejareja za bidhaa za mafuta kwa Mikoa ya Kaskazini zimebadilika ikilinganishwa na toleo la tarehe 4 Aprili 2018. Katika toleo hili la Mei 2018, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa Mikoa ya Kaskazini zimeongezeka kwa Shilingi 3/lita (sawa na asilimia 0.14) na Shilingi 15/lita (sawa na asilimia 0.71). Aidha, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli zimepungua kwa Shilingi 9.81/lita (sawa na asilimia 0.46) wakati bei za jumla za Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 1.96/lita (sawa na asilimia 0.10). Kutokana na mkoa wa Tanga kuishiwa Mafuta ya Taa, wamiliki wa vituo vya mafuta katika Mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kununua mafuta hayo Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini zitatokana na gharama za mafuta hayo yaliyopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa hadi Mikoa ya Kaskazini.
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa

taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (e) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163/2018 la mwezi April 2018.****
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (g) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

#### A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>2,227</b>	<b>2,145</b>	<b>2,156</b>
<b>Arusha</b>	<b>2,282</b>	<b>2,186</b>	<b>2,240</b>
Arumeru (Usa West)	2,282	2,186	2,240
Karatu	2,300	2,204	2,258
Monduli	2,287	2,191	2,246
Monduli-Makuyuni	2,292	2,196	2,250
Ngorongoro (Loliondo)	2,366	2,270	2,332
<b>Kibaha</b>	<b>2,232</b>	<b>2,149</b>	<b>2,161</b>
Bagamoyo	2,239	2,156	2,167
Kisarawe	2,235	2,152	2,163
Mkuranga	2,237	2,155	2,166
Rufiji	2,255	2,172	2,184
<b>Dodoma</b>	<b>2,286</b>	<b>2,204</b>	<b>2,215</b>
Bahi	2,294	2,211	2,222
Chemba	2,313	2,230	2,241
Kondoa	2,319	2,236	2,248
Kongwa	2,284	2,201	2,212
Mpwapwa	2,287	2,205	2,216
<b>Iringa</b>	<b>2,292</b>	<b>2,209</b>	<b>2,220</b>
Kilolo	2,296	2,213	2,225

Mufindi (Mafinga)	2,302	2,219	2,230
<b>Njombe</b>	<b>2,320</b>	<b>2,237</b>	<b>2,248</b>
Njombe (Kidegembye)	2,341	2,258	2,269
Ludewa	2,358	2,275	2,286
Makete	2,351	2,268	2,279
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,318	2,235	2,246
<b>Bukoba</b>	<b>2,443</b>	<b>2,360</b>	<b>2,372</b>
Biharamulo	2,417	2,335	2,346
Karagwe (Kayanga)	2,459	2,377	2,388
Kyerwa (Ruberwa)	2,465	2,382	2,394
Muleba	2,443	2,360	2,372
Ngara	2,408	2,326	2,337
Misenyi	2,451	2,369	2,380
<b>Geita</b>	<b>2,393</b>	<b>2,310</b>	<b>2,321</b>
Bukombe	2,382	2,299	2,310
Chato	2,414	2,331	2,343
Mbogwe	2,431	2,348	2,360
Nyang'hwale	2,408	2,325	2,336
<b>Kigoma</b>	<b>2,459</b>	<b>2,376</b>	<b>2,387</b>
Uvinza (Lugufu)	2,471	2,388	2,400
Buhigwe	2,448	2,365	2,377
Kakonko	2,416	2,333	2,345
Kasulu	2,445	2,362	2,373
Kibondo	2,423	2,340	2,352
<b>Moshi</b>	<b>2,271</b>	<b>2,175</b>	<b>2,230</b>
Hai (Bomang'ombe)	2,275	2,178	2,233
Mwanga	2,264	2,168	2,223
Rombo (Mkuu)	2,288	2,192	2,251
Same	2,258	2,162	2,216
Siha (Sanya Juu)	2,278	2,182	2,236
<b>Lindi</b>	<b>2,286</b>	<b>2,204</b>	<b>2,215</b>
Lindi-Mtama	2,304	2,222	2,233
Kilwa Masoko	2,261	2,179	2,190
Liwale	2,307	2,225	2,236
Nachingwea	2,316	2,233	2,244
Ruangwa	2,317	2,235	2,246
<b>Babati</b>	<b>2,316</b>	<b>2,220</b>	<b>2,278</b>
Hanang (Katesh)	2,326	2,230	2,289
Kiteto (Kibaya)	2,331	2,235	2,289
Mbulu	2,328	2,232	2,291
Simanjiro (Orkasumet)	2,348	2,252	2,310
<b>Musoma</b>	<b>2,406</b>	<b>2,323</b>	<b>2,335</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,447	2,364	2,375
Rorya (Ingirijuu)	2,415	2,332	2,344
Rorya (Shirati)	2,450	2,367	2,378
Bunda	2,397	2,315	2,326
Butiama	2,403	2,320	2,331
Serengeti (Mugumu)	2,452	2,369	2,380

Tarime	2,417	2,334	2,346
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,422	2,339	2,350
<b>Mbeya</b>	<b>2,335</b>	<b>2,252</b>	<b>2,263</b>
Chunya	2,344	2,261	2,273
Chunya (Makongolosi)	2,358	2,276	2,287
Ileje	2,348	2,265	2,276
Kyela	2,350	2,268	2,279
Mbarali (Rujewa)	2,319	2,236	2,247
Mbozi (Vwawa)	2,344	2,261	2,272
Momba (Chitete)	2,353	2,270	2,281
Rungwe (Tukuyu)	2,344	2,261	2,272
<b>Morogoro</b>	<b>2,252</b>	<b>2,170</b>	<b>2,181</b>
Mikumi	2,268	2,185	2,197
Kilombero (Ifakara)	2,290	2,208	2,219
Kilombero (Mlimba)	2,313	2,230	2,241
Kilombero (Mngeta)	2,302	2,219	2,230
Ulanga (Mahenge)	2,301	2,218	2,230
Malinyi	2,311	2,229	2,240
Kilosa	2,271	2,188	2,199
Gairo	2,271	2,188	2,199
Mvomero (Wami Sokoine)	2,263	2,180	2,191
Turiani	2,278	2,195	2,206
<b>Mtwara</b>	<b>2,300</b>	<b>2,217</b>	<b>2,228</b>
Nanyumbu (Mangaka)	2,349	2,266	2,277
Masasi	2,326	2,243	2,254
Newala	2,332	2,249	2,261
Tandahimba	2,325	2,242	2,254
<b>Mwanza</b>	<b>2,378</b>	<b>2,295</b>	<b>2,306</b>
Kwimba	2,414	2,331	2,342
Magu	2,386	2,303	2,314
Misungwi	2,383	2,301	2,312
Sengerema	2,410	2,327	2,339
Ukerewe	2,437	2,354	2,366
<b>Sumbawanga</b>	<b>2,400</b>	<b>2,318</b>	<b>2,329</b>
Kalambo (Matai)	2,408	2,325	2,336
Nkasi (Namanyeke)	2,414	2,331	2,343
<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>2,436</b>	<b>2,353</b>	<b>2,364</b>
Mlele (Inyonga)	2,414	2,331	2,342
Mpimbwe (Majimoto)	2,428	2,345	2,356
<b>Songea</b>	<b>2,351</b>	<b>2,268</b>	<b>2,279</b>
Mbinga	2,385	2,302	2,313
Namtumbo	2,380	2,298	2,309
Nyasa (Mbamba Bay)	2,387	2,304	2,315
Tunduru	2,410	2,327	2,338
<b>Shinyanga</b>	<b>2,356</b>	<b>2,274</b>	<b>2,285</b>
Kahama	2,370	2,287	2,299
Kishapu	2,385	2,302	2,313
Simiyu (Bariadi)	2,398	2,315	2,326

Busega (Nyashimo)	2,391	2,308	2,319
Itilima (Lagangabilili)	2,401	2,318	2,329
Maswa	2,389	2,307	2,318
Meatu (Mwanhuzi)	2,396	2,314	2,325
<b>Singida</b>	<b>2,318</b>	<b>2,236</b>	<b>2,247</b>
Iramba	2,330	2,248	2,259
Manyoni	2,303	2,220	2,231
Ikungi	2,314	2,231	2,242
Mkalama (Nduguti)	2,343	2,260	2,271
<b>Tabora</b>	<b>2,382</b>	<b>2,299</b>	<b>2,310</b>
Igunga	2,336	2,253	2,264
Kaliua	2,400	2,317	2,328
Ulyankulu	2,394	2,311	2,322
Nzega	2,346	2,264	2,275
Sikonge	2,394	2,311	2,322
Urambo	2,395	2,312	2,323
<b>Tanga</b>	<b>2,225</b>	<b>2,129</b>	<b>2,202</b>
Handeni	2,246	2,150	2,182
Kilindi	2,261	2,165	2,216
Korogwe	2,237	2,141	2,195
Lushoto	2,246	2,150	2,205
Mkinga (Maramba)	2,232	2,136	2,216
Muheza	2,230	2,134	2,202
Pangani	2,232	2,136	2,209

**B: BEI ZA JUMLA**

<b>Bei za Jumla – DSM</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,103.47</b>	<b>2,020.66</b>	<b>2,032.45</b>

<b>Bei za Jumla – TANGA</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,101.01</b>	<b>2,004.89</b>	<b>1,816.24</b>

**Nzinyangwa E. Mchany**  
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**